

# **KISHAZI HURU ARIFU CHA KISWAHILI: MTAZAMO WA X-BAR**

**NA**

**PRISCA JERONO**

Tasnifu hii imetolewa kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya

Shahada ya Uzamili (M.A)  
Katika Chuo Kikuu cha Nairobi



**SEPTEMBER 2003**


## **UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mimi mwenyewe na hajatolewa na mtu ye yote kutosheleza mahitaji ya digrii katika Chuo Kikuu kingine.



**PRISCA JERONO**

Tasnifu hii imetolewa kwa utahini kwa idhini yangu kama msimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.



**PROF.M. H. ABDULAZIZ**

## **TABARUKU**

**Tasnifu hii nawatabarukia marehemu nyanyangu,  
Ruth Kimoi na wanangu Trevor Kiprop  
na Carleen Jepkurui**

# **YALIYOMO**

UNGAMO .....	ii
TABARUKU .....	iii
SHUKRANI .....	vi
DHAHANIA .....	vii
ORODHA YA VIFUPISHO NA ISHARA .....	viii
<b>SURA YA KWANZA</b>	
1.1 UTANGULIZI .....	1
1.2 MADA YA UTAFITI .....	1
1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI .....	2
1.4 NADHARIA TETE .....	3
1.5 UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU .....	3
1.6 SABABU ZA KUCHAGUA MADA .....	4
1.7 MSINGI WA KINADHARIA .....	4
1.8 UDURUSU WA YALIYOANDIKWA .....	14
1.9 NJIA ZA UTAFITI .....	19
<b>SURA YA PILI</b>	
2.1 KATEGORIA .....	20
2.2 VIRAI .....	20
2.2.1 VIRAI VYA KILEKSIKA .....	21
2.2.1.1 Virai Nomino .....	21
2.2.1.2 Virai Vumishi .....	25
2.2.1.3 Virai Elezi .....	27
2.2.1.3.1 Virai elezi vya namna .....	27
2.2.1.3.2 Virai elezi vya wakati .....	28
2.2.1.3.3 Virai elezi vya mahali .....	28
2.2.1.3.4 Virai elezi viulizi .....	29
2.2.1.3.5 Virai elezi vya kiasi .....	30
2.2.4 Virai tenzi .....	30
2.2.5 Virai husishi .....	33
2.3 KATEGORIA ZA KIUAMILIFU .....	34
2.3.1 KIIMA .....	34
2.3.2 KIARIFU .....	35
2.3.3 YAMBWA .....	36

2.3.4 KIBAINISHI.....	36
2.3.5 KIJALIZI .....	37
2.3.6 KIAMBAJENG CHA MNYAMBULIKO (M) .....	37
2.3.6.1 KIRAI KIPATANISHI (Kp).....	38
2.3.6.2 KIRAI CHA YAMBWA (Ky).....	43
2.3.6.3 KIRAI CHA NJEO (Kn).....	43
<b>SURA YA TATU</b>	
3.1 MUUNDO WA KISHAZI HURU.....	48
3.1.1 Kishazi huru chenye kitenzi kisoelekezi .....	51
3.1.2 Kishazi huru chenye kitenzi elekezi.....	53
3.1.3 Kishazi kisicho na kiima .....	55
3.1.4 Kishazi kilicho na kirai husishi .....	57
3.1.5 Kishazi chenye kitenzi kishirikishi .....	58
<b>SURA YA NNE</b>	
4.1 HITIMISHO.....	62
4.2 MAPENDEKEZO.....	63
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>65</b>

## **SHUKRANI**

Ningependa kuchukua fursa hii kwanza kutoa shukrani zangu kwa msimamizi wangu Prof. M. H. Abdulaziz ambaye hakuchoka kuipitia kazi hii pamoja na ushauri wake mkuu ambao ulinitia moyo na kuniwezesha kuona upya vipengele mbalimbali katika utafiti wangu.

Pili shukrani zangu ziendee Idara na Chuo kwa ufadhilli wao ambao uliniwezesha kuendelea na masomo yangu bila kutatizika.

Tatu shukrani nyingi zimwendee Dkt. Mwenda Mbatia ambaye amekuwa msaidizi wangu katika kunifunza mengi yanayohusiana na taaluma hii ya uandishi. Ushirikiano wangu naye umeniwezesha kufahamu mengi ambayo yatanifaa katika maisha yangu.

Nne, mwalimu Mgullu ambaye aliweza kunipa changamoto ya kufanya utafiti huu kuitia mafunzo mengi aliyonipa darasani. Vilevile nawashukuru walimu wengine ambao walisaidia nilipotaka ushauri wao. Hawa ni pamoja na Dkt. Alfred Buregeya, Mwalimu Oloo na Mwalimu Arege.

Ningependa vilevile kuwashukuru wazazi wangu Alfred na Hellen ambao daima walinitia moyo kuyaendeleza masomo yangu, mume wangu Richard na wanangu Trevor na Carleen ambao iliwabidi kunikosa wakati nilipokuwa nikishughulika na masomo yangu.

Siwezi kuwasahau wenzangu tuliodurusu nao kwa kunitia moyo, ushauri wao pamoja na ucheshi wao ulioufanya mkondo huu kuwa mfupi. Hawa ni pamoja na Grace, Gakero, Muhati, Kamau, Magare, Amadi, Omwenga Bwire, Nzuki, Osoro, Elizabeth na Suzy.

Kwenu nyote nasema ahsanteni sana na baraka za Mungu ziwashukie.

## DHAHANIA

Tasniifu hii inajaribu kuonyesha miundo ya virai na vishazi huru nya Kiswahili kwa mujibu wa nadharia ya X-bar kwa madhumuni ya kuonyesha namna ambavyo nadharia hii inavyoweza kutumika kuonyesha miundo ya virai na vishazi pamoja na nafasi ya vipashio mbalimbali katika miundo hii.

Katika sura ya kwanza tumeangaza kuhusu utangulizi mfupi wa nadharia ya X-bar na kueleza mada ya utafiti. Vilevile tumeangalia madhumuni ya utafiti, nadharia tete, msingi wa kinadharia, udurusu wa kazi mbalimbali pamoja na njia za utafiti.

Katika sura ya pili tumeangazia kuhusu dhana ya kategoria na kategoria mbalimbali zinazotumika katika uundaji wa virai. Vilevile tumeeleza kuhusu dhana ya virai na kuonyesha virai mbalimbali vinavyotumika katika uundaji wa vishazi huru pamoja na miundo yao.

Katika sura ya tatu tumeonyesha uchanganuzi wa miundo ya vishazi huru kwa mujibu wa nadharia hii ya X-bar. Katika uchanganuzi huu tumezingatia miundo ya virai vilivyoonyeshwa katika sura ya pili. Vilevile kuna maelezo machahe kuhusiana na vishazi huru na vipashio mbalimbali vinavyotumika katika uundaji wa vishazi huru.

Sura ya nne inatoa mahitimisho kuhusiana na uchanganuzi wa muundo wa kishazi huru pamoja na mapendekezo kuhusiana na utafiti zaidi katika eneo hili.

## **Orodha ya Vifupisho na Ishara**

S	Kishazi
KB	Kibainishi
KT	Kirai tenzi
KN	Kirai nomino
'	Bar moja
M	Kategoria ya mnyambuliko inayowakilisha njeo na vipatanishi
p	Kipatanishi
n	Njeo
KE	Kirai elezi
E	Kielezi
T	Kitenzi
N	Nomino
X	Kiwakilishi cha kategoria yoyote
KX	Kirai kamili cha kategoria yoyote
J	Kijalizi kinachotanguliza kishazi
KJ	Kirai jalizi
<i>X-bar</i>	Nadharia kuhusu uwakilishi wa virai
PRO	Kiima cha kishazi kisoukomodo
pro	Kiwakilishi cha kiima kilichoachwa
{ }	Mofu
Kp	Kirai Kipatanishi
Kn	Kirai njeo
Ø	Kategoria kapa

	<b>Bar mibili</b>
<b>Ky</b>	<b>Kirai Yambwa</b>
<b>KH</b>	<b>Kirai husishi</b>
<b>H</b>	<b>Kihuishi</b>
<b>W</b>	<b>Kiwakilishi</b>
<b>Kv</b>	<b>Kirai vumishi</b>
<b>V</b>	<b>Kivumishi</b>
<b>y</b>	<b>yambwa</b>

## 6.2 MUDIA YA UTAFI

Utafiti ya mudia ya utafii ni kifaa kila kiswahili wa kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili.

Utafiti ya mudia ya utafii ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili.

Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili. Kisiwa hili ni kifaa kila kiswahili na kifaa kila kiswahili.

# **SURA YA KWANZA**

## **1.1 UTANGULIZI**

Utafiti huu unachunguza muundo wa kishazi huru cha Kiswahili Sanifu kwa kutumia nadharia ya *X-bar*. Nadharia hii ni tawi mojawapo la nadharia pana ya Umilikifu na Masharti (UM). Hii ni nadharia inayotumiwa katika kuchunguza ubia wa sarufi za lugha. Sarufi ni mfumo wa kaida ambazo hutumika katika uundaji wa vipashio vya lugha kama vile sentensi. Kwa sababu nadharia hii ni ya kisasa, tumeitumia kuchunguza katika miundo ya vishazi huru vya Kiswahili ili kubainisha ubia wake.

## **1.2 MADA YA UTAFITI**

Utafiti huu unanuia kuonyesha muundo wa kishazi huru arifu cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya *X-bar*. Hili tawi mojawapo la nadharia zinazotumiwa kuchunguza viambajengo mbalimbali vya lugha katika Nadharia Panuzi ya Umilikifu na Masharti.

Tawi hili la *X-bar* linatumika katika kuchunguza miundo ya virai. Katika nadharia hii ya *X-bar* kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini kisicho na muundo wa kiima na kiarifi (TUKI :1990) Mifano ya virai ni kama vile:

Kirai nomino (KN)-Mtoto mzuri

Kirai vumishi (KV)-kizuri sana

Kirai elezi (KE)-jana jioni

Kirai tenzi (KT)-njoo hapa

Kirai husishi (KH)-kwa mkutano

Kutokana na miundo ya virai tunaweza kuchunguza miundo ya vipashio vikubwa kama vile vishazi kwa sababu kama asemavyo Radford (1997:62) virai na vipashio vingine vikubwa huundwa kwa njia ya muungano. Njia ya muungano inatumika katika uundaji wa

vipashio vikubwa kwa kuunganisha kategoria mbili au zaidi ili kuunda ~~virai na virai~~  
~~vishazi~~ au ~~zaidi ili kuunda~~ vishazi. Katika nadharia hii kategoria hurejelea aina mbalimbali za maneno ya kisarufi kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, vihusishi, vielezi na aina za maneno ya kiuamilifu kama vile vibainishi, vijalizi na vijalizo.

Kwa kuzingatia njia hii ya muungano tumeonyesha miundo ya vishazi vinavyotokana na kuunganisha virai mbalimbali vinavyoundwa kutokana na kategoria hizi za manaeno.

Kumekuwa na tafiti nyingi kuhusu miundo ya virai mbalimbali kwa kutumia nadharia ya *X-bar* na tumeonelea kwamba inafaa tuchangie tafiti hizi kwa kuchunguza muundo wa kishazi huru arifu. Tafiti nyingi zimejikita katika miundo ya virai hasa kirai nomino. lakini utafiti wetu utaonyesha miundo ya virai vingine vinavyounda vishazi huru vikiwemo virai nomino, elezi, husishi, vitenzi, vumishi, vijalizi na vya myambuliko.

Tunaturmaji kwamba utafiti huu utatupa mwanga zaidi kuhusu matumizi ya nadharia ya Sarufi Bia kuichunguza lugha ya Kiswahili.

### 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti wetu una madhumuni yafuatayo:

1. Kubainisha muundo wa kishazi huru arifu cha Kiswahili Sanifu kwa mujibu wa nadharia ya *X-bar*. Tumefanya hivi kwa kuchambua viambajengo vyake mbalimbali na hasa kategoria zake za kiuamilifu za vijalizi na viambishi awali vya myambuliko katika vitenzi pamoja na nafasi yake katika muundo wa kishazi.
2. Kuonyesha miundo ya virai vya Kiswahili Sanifu kwa mujibu wa nadharia ya *X-bar*. Kwa kuchambua muundo wa kishazi tutaweza kuonyesha miundo ya virai

vinavyounda vishazi kwa kuchukulia kwamba vishazi vinaundwa kwa njia sawa ya muungano ya kuunganisha virai mbalimbali.

## 1.4 NADHARIA TETE

Utafiti huu umefanywa katika misingi ya nadharia tete zifuatazo:

- (i) Viambishi vya upatanishi, njeo na yambwa vinaweza kuwa na miundo ya virai kamili kwa kuambatana na nadharia ya *X-bar*.
- (ii) Kifungutenzi cha Kiswahili kinabeba kiima cha kirai. Kufuatana na nadharia ya *X-bar*, kifungutenzi cha kiswahili ni ile sehemu ya kishazi inayotoa uarifu wa kiima.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU

Utafiti wetu umejikita katika kuchunguza kishazi huru cha Kiswahili Sanifu na hautaingilia vishazi tegemezi. Vishazi ambavyo vimeshughulikiwa vimehusisha virai vya kileksika na virai vya kiuamilifu.

Utafiti wetu vilevile umejikita katika nadharia ya *X-bar* na hatujashughulika na matawi mengine ya nadharia ya Umilikifu na Masharti.

Mbali na hayo kazi yetu haijashughulika na uhamisho unaofanyiwa viambajengo vya vishazi huru hivyo utafiti wetu umejikita katika umbo lake zalika, yaani umbo la vishazi vya kawaida.

Pale ambapo imetulazimu tumetumia kitengo cha Mofoloja katika kuchanganua vipengele vya kirai cha mnyambuliko (KM) yaani mofu za upatanishi, njeo, na yambwa ila hatujaingilia kitengo hiki kwa undani.

Pamoja na hayo, utafiti wetu umechambua virai ambavyo vimeatumika kuunda vishazi huru.

## 1.6 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Tumeichagua mada hii kwa sababu uchunguzi wetu wa awali haukuweza kupata kuona utafiti uliowahi kufanywa juu ya vishazi huru vya Kiswahili Sanifu kwa kutumia nadharia ya *X-bar*. Aidha changanuzi za virai ambazo zimefanywa kwa kutumia nadharia hii zimejikita katika virai nomino, lakini utafiti wetu umechangana aina zingine za virai vikiwemo virai husishi, elezi vitenzi na vumishi

Sababu nyingine ya kuichagua mada hii inatokana na umuhimu wa kutumia nadharia ya kisasa, yaani *X-bar*, katika kuchunguza vipengele mahsusvi vya lugha ya Kiswahili.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Nadharia hii ambayo tumeitumia katika utafiti wetu wa kuchunguza muundo wa kishazi huru cha Kiswahili Sanifu inahusu kaida za mpangilio wa viambajengo vya virai. Nadharia hii ya *X-bar* iliasisiwa na Jackendoff R. na kuendelezwa na Chomsky katika jaribio la kuonyesha miundo ya virai vya lugha. Pamoja na nadharia hii Chomsky pia aliunda Nadharia ya Sarufi Bia ambayo inabainisha sifa bia za sarufi ya kila lugha. Nadharia hii ya *X-bar* inayotumika kuelezea miundo ya virai vya kila lugha ni miongoni mwa nadharia zinazotumika kuunda nadharia ya Sarufi Bia.

Nadharia hii ya *X-bar* ilitokana na upungufu ulioonekana kuwepo katika nadharia ya Sarufi Miundo Virai. Nadharia hii ya Sarufi Miundo Virai ilikuwa na kanuni nyingi zilizohusisha kategoria mbalimbali katika uwakilishi wa miundo ya sentensi. Nadharia ya *X-bar* hivyo basi ilizuka kama suluhisho la upungufu huu kwani kama asemavyo


Newmeyer (1986:152-153) nadharia ya *X-bar* ilibadilisha kanuni za miundo virai kwa kutumia ishara hizi:

$X'' \longrightarrow [kibainishi cha X'] X'$

$X' \longrightarrow X\dots$


Kwa kufanya hivi kategoria zote zimekuja kuwakilishwa kwa ishara moja hivyo kuondolea mbali umuhimu wa kategoria. Aidha kinyume na nadharia ya Sarufi Miundo Virai nadharia hii inaonyesha mahusiano ya ndani ya vipengele mbalimbali vya virai.

Katika nadharia hii ya *X-bar* kuna kaida za mvurumisho wa kategoria za virai kutoka kwa kategoria leksika pamoja na masharti ya mpangilio wa kiwima wa kategoria katika muundo wa kielelezo kifuatacho:




(Horrocks 1987:64)

Kwa mfano kirai nomino '*Huyu mtoto wangu*' utakuwa na muundo:




Kategoria X hubadilika ili kuwakilisha kategoria zote za kileksika yaani nomino, vitenzi, vivumishi, vihusishi na vielezi. X ni mvurumisho wa bar moja wa kichwa X na X\* ni *bar* mbili ama uvurumisho wa juu kabisa wa kitengo X. X inatoa tafsili ya vijalizo na chagizo cha kichwa X. Kijalizo ni aina ya neno ambalo hukamilisha maana hasa katika vitenzi vishirikishi. Vijalizo vingi hutokana na nomino, viwakilishi na vivumishi. Chagizo ni aina ya neno ambalo linaweza kuondolewa katika muundo wa kirai na kirai hicho kikaweza kujisimamia. Chagizo ni kategoria ambayo hutumika kuelezea vile vipashio vyta kuelezi ambavyo mara nyingi huwa vielezi na vihusishi. Katika nadharia hii kuna dhana ya kichwa cha kirai ambacho ni ile kategoria inayotawala fungu la maneno. Kichwa cha kirai kinaweza kuwa mwanzoni ama mwishoni mwa kifungu kinachounda mvurumisho wa bar moja kwa kutegemea lugha husika. Kiswahili ni lugha iliyio na nafasi ya kichwa mwanzoni. Vijalizo pamoja na vibainishi ni muhimu katika mvurumisho wa hali ya juu kabisa wa kirai.

Kufuatana na maendeleo ya kinadharia vichwa vinavyosimama bila vibainishi au vijalizo vimekuja kuchukuliwa kuwa virai kamili kutokana na haja ya kubana nadharia hii ili kuweza kutumika kuwakilisha miundo mbalimbali. Kutokana na hali hii nafasi hizi huchukuliwa kuwa kapa pale ambapo hazijazwa. Vilevile vipashio vingine vidogo kama vile mofu huchukuliwa kama virai kamili (Ouhala 1991:52). Kwa mfano katika kirai *huyu mtoto mzuri*, kategoria mtoto huvurumishwa kwa bar moja kwa kuongezwa kijalizo mzuri na huvurumishwa zaidi katika bar mbili kwa kuongezwa kibainishi huyu. Katika mfano huu kichwa cha kirai hiki ni nomino hivyo kuwa kirai nomino. Kwa mfano:



Wakati kirai hiki hakina kijalizo na kibainishi hakipo kirai hiki huwa na muundo ufuatao:



Kulingana na nadharia hii kirai ndicho kiambajego muhimu. Kamusi ya TUKI (1990) inasema 'kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima kiarifu. Nadharia hii awali ilitumika katika kuonyesha miundo ya virai pekee vilivyoundwa kutokana na kategoría za kisarufi kama vile: nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na vihusishi lakini baadaye virai vya kategoría za kiuamilifu kama vile vibainishi, kiima, yambwa, vijalizi na viambishi awali vya mnyambuliko katika vitenzi vikaingizwa katika nadharia hii ili kuleta usawazisho wa kimuundo. Kutokana na hali hii vipashio vidogo kama vile mofu ambavyo ni viambishi vinavyopachikwa kwenye vitenzi vimeweza kuainishwa katika kategoría ya virai. Aidha vipashio vikubwa kama vile vishazi vimeweza kuchunguzwa kwa kutumia nadharia hii kwaani vipashio hivi huundwa kwa kuunganisha vipashio vidogo kama vile virai kwa njia ya muungano (Radford 1997:62). Kutokana na hali hii tumeweza kuchunguza muundo wa kishazi Mohamed (2001: 227) anasema kuwa kwa kijumla kishazi huundwa kutokana na kiima na kiarifu nao Massamba na wengine (1999: 115) wanasema kuwa kishazi ni kundi la


maneno lenye kiima na kiarifu hasa likiwa ndani ya sentensi kuu. Kutokana na tafsili hizi kishazi hivyo basi huwa na kiima na kiarifu.

Maendeleo haya ya kinadharia yamepelekea kuhusishwa kwa kategoria za kiuamilifu za kijalizi J, ambacho hutanguliza vishazi na kitengo cha mnyambuliko KM ambacho huambishwa kwenye vitenzi. Kufuatana na haya, vishazi huru vimeelezwa kuwa:

Vishazi vyote vya kawaida vina muundo wa kiambajengo *S-bar* ulio na muundo wa kielelezo [J S] na hivyo kuwa na kiambajengo J ambacho kinaweza kuwa kimejazwa (kwa mfano na vijalizo ama vitenzi visaidizi vilivyofanyiwa mageuzi) ama kilichoachwa wazi. Radford (1988: 301) (Tafsiri yetu).

Katika nadharia hii muundo wa kishazi umeonekana kuwa wenyе viambajengo J S ambapo J huchukuliwa na kijalizo cha kitenzi, nomino, vivumishi au kategoria nyiningine ilhali S ambayo ni kishazi huwa na muundo wa KN M-bar. Katika muundo huu KN ni nafasi ya kirai nomino ambacho ni kibainishi cha M-bar. Nafasi ya kirai nomino hiki katika muundo wa kishazi huchukuliwa na kiima cha kishazi M ni nafasi inayochukuliwa na viambishi vya mnyambuliko vinavyowakilisha vipatanishi, njeo, hali, ukarusho na yambwa, urejelezi na kadhalika. Hivyo muundo wa kishazi umeonekana kuwa na muundo ufuatao:

KJ




(Ouhalia 1991:28 Tafsiri yetu)

Katika muundo huu M ni nafasi inayochukuliwa na viambishi awali vyatanya mnyambuliko wa kitenzi kama vile: njeo, hali, upatanisho na kadhalika. Muungano wa kirai tenzi pamoja na viambishi hivi hufanyika kupitia uhamisho wa kitenzi hadi M. Katika lugha ya Kiswahili kiambajengo hiki huambishwa kwenye vitenzi na pamoja na kijalizo chake ambacho ni kitenzi, huunda M-bar. Kiambishi hiki cha M kulingana na Ouhalia (1991:56) hubeba viambishi vyatanya vipengele mbalimbali wala haihusishwi na kategoria moja mahsusini. Hali hii hivyo basi huenda kinyume na kaida ya *X-bar* ambayo inahitaji kuonyesha uwakilishi wa muundo wa kategoria moja mahsusini. Ili kuleta usawazisho wa kiuwakilishi hali hii imesababisha kuzuka kwa nadharia tete ya kukivunja kitengo hiki katika vichwa mbalimbali yaani (*Split INFL Hypothesis*) na kupelekea virai kuhusishwa na vipashio vidogo kama vile mofu. Kitengo hiki huvunjwa katika viambishi mbalimbali ambavyo kila moja hutawala mvurumisho wake (Ouhalia 1991:52).


Miongoni mwa viambishi hivi ni vyatanya njeo, vipatanishi, hali, yambwa na ukarusho ambavyo vimechukuliwa kuwa virai kamili vilivyo na vichwa mbalimbali yaani kirai kipatanishi (Kp), kirai njeo (Kn), kirai yambwa (Ky), kirai kanushi (Ko) na kirai hali (Kl).

Kutokana na haya, utafiti wetu umejikita katika virai vitatu yaani kirai njeo (Kn), kirai kipatanishi (Kp) na kirai yambwa (Ky). Ouhalia (kama hapo juu) anaendelea kusema kwamba mpangilio wa viambajengo hivi hutofautiana kwa kutegemea aina ya lugha inayohusika. Lugha ya Kiswahili ambayo ni aina ya lugha yenyewe mpangilio wa Kiima, Kiarifu na Yambwa(SVO) huwa na mpangilio wenye kirai njeo kinachokuja baada ya kirai kipatanishi. Kirai yambwa hujitokeza katika nafasi kabla ya mzizi wa kitenzi. Hivyo muundo wa kiambajengo hiki cha M utakuwa kama ifuatavyo:




Yambwa (y) inapouunganishwa na kirai tenzi (KT) huunda mvurumisho wa bar moja yaani y' na inapouunganishwa na kibainishi chake huunda kirai kamili chenye mvurumisho wa bar mbili yaani Ky. Njeo (n) inapouunganishwa na kirai yambwa (Ky) huunda mvurumisho wa bar moja yaani n', na inapouunganishwa na kibainishi chake huunda kirai kamili chenye mvurumisho wa bar mbili yaani Kn. Kipatanishi (p) kinapouunganishwa na kirai njeo (Kn) huunda mvurumisho wa bar moja yaani p' na inapouunganishwa na kibainishi chake huunda kirai kamili chenye mvurumisho wa bar mbili yaani Kp.

Kibainishi hiki cha Kp huchukuliwa na kiima cha kishazi yaani KN kwa kuambatana na kaida ya vibainishi ambayo huhitaji kibainishi kuwa na upatanisho baina yake na kichwa chake. Kiima katika Kiswahili huwa na upatanishi wa kisarufi na kipatanishi chake hivyo kukalia nafasi hii. Hata hivyo wakati mwagine nafasi hii inaweza kuwa hajajazwa kutokana na hali kwamba vipatanishi huweza huwakilisha kiima katika lugha ya Kiswahili. Nafasi hii hivyo basi huwakilishwa na kifupisho *pro* kwa kuambatana na kigezo cha baadhi ya matumizi ya lugha kuacha kuonyesha kiima cha kishazi na *PRO* ili kuonyesha nafasi ya kiima cha kishazi kisoukomo ambayo huwa wazi kama asemavyo Ouhalia (1991:30-31). Kutokana na hali hii vishazi vitakuwa na muundo ufuata:



Kila mojawapo wa vishazi hivi huwa na muundo wa JS ambapo S hapa ni kishazi kinachotangulizwa na Kp ilhali J ni kijalizi. Kijalizi pamoja na Kp huunda J' na kutokana na kaida ya *X-bar* kirai kamili huundwa kwa mvurumisho wa bar mbili. Hivyo J' huongezwa kibainishi (KB) ambacho ni muhimu katika mvurumisho wa bar mbili ili kuunda KJ. Vijalizi hivi vinaweza kuwa vimejazwa au kuwa kapa Katika lugha zingine

nafasi hii huchukuliwa na virai vya maswali lakini katika lugha ya Kiswahili nafasi hii haijajazwa hivyo kuwa kapa. Vishazi huru hivyo basi vitakuwa na muundo ufuatao:




(Radford 1988: 512, Tafsiri yetu)

Kwa mfano katika sentensi 'Juma alisema kuwa Maria ataenda nyumbani' kuna vishazi viwili yaani:

- (i) Juma alisema
- (ii) Maria ataenda nyumbani.

Kijalizo cha J hapa ni neno *kuwa*. Kishazi kinachotangulizwa na kijalizi hiki ni kishazi tegemezi ilhali kile kinachokuja kabla ya kijalizi ni kishazi huru. Kila mojawapo ya vishazi hivi kina muundo wa *S-bar* wenye kielelezo J S hivyo muundo wake utakuwa:



Katika uwakilishi huu wetu tumetumia pembe tatu kuonyesha miundo ambayo hatujakamilisha kutokana na sababu za kinafasi.

## 1.8 UDURUSU WA YALIYOANDIKWA

Udurusu wetu ulihusisha kazi za aina mbili: Kwanza tulidurusu kazi ambazo zinahusika na sintaksia ya lugha ya Kiswahili na pili kuna zile kazi zinazohusika na nadharia ambayo tumeitumia. Kazi ambazo zimepitiwa ni zile zinazohusika na vipengele mbalimbali nya kimuundo katika lugha ya Kiswahili. Kazi hizi ni zile zilizoandikwa bila kuzingatia nadharia yoyote. Mifano ni kama vile Broomfield (1931), *Sarufi ya Kiswahili*, Loogman (1965), *Swahili Grammar and Syntax* na Ashton (1944), *Swahili Grammar Including Intonation*.

Polome (1967) katika *Swahili Syntax* ametoa maeleo kuhusu sarufi ya Kiswahili. Yaliyotufaa katika utafiti wetu ni maeleo kuhusu virai, vishazi na viambishi nya njeo, vipatanishi na ukusho.

Mohamed (2001) katika *Modern Swahili Grammar* ametufaa kwa maeleo kuhusu uanisho wa ngeli, viambishi nya kiambajengo cha M na fasili kuhusiana na vishazi nya Kiswahili.

Kihore na wengine (2001) katika *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* wametufaa katika maeleo yao kuhusu kategoria mbalimbali za maneno, viambishi nya vitenzi vikiwemo vile nya njeo, vipatanishi, nya nafsi na yambwa. Viambishi hivi vimetumika katika kufafanua viambishi nya kitengo cha M. Aidha ametuelezea kuhusu uainisho wa ngeli za Kiswahili.

Massamba na wengine (1999) katika *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* wametufaidi katika kuainisha virai vya Kiswahili japo walijikita katika kanuni miundo virai ilio katika nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo Warneeleza kuhusu viambajengo vya virai vya Kiswahili Mbali na hayo wameonyesha tofauti iliyopo baina ya vishazi huru na vishazi tegemezi.

Mkude (1983) katika *Uchambuzi wa Sentensi za Kiswahili* anaeleza kuhusu fasili ya vishazi na viambajengo vinavyounda virai mbalimbali. Virai hivi huunda vishazi mbalimbali

Kamau (2001) Katika *Sintaksia ya Virai vya Kiswahili Sanifu na Kikikuyu cha Kabete* ameshughulikia kirai nomino cha Kiswahili na Kikikuyu kiulinganishi. Japo alitumia nadharia tofauti na yetu ametufaa pakubwa kwa kuonyesha vipengele vyote vinavyounda virai nomino, virai husishi na virai elezi.

Olali (1997) ameshughulikia *Kikundi Nomino cha Kiswahili Sanifu katika Mtazamo wa X-bar*. Kazi yake ni muhimu kwetu kwani imetupa mwangaza kuhusu muundo wa kirai nomino katika mtazamo wa *X-bar*. Vilevile ametufaa kwa kutuangazia kuhusu nadharia zinazounda nadharia ya UM pamoja na istilahi za nadharia hii katika lugha ya Kiswahili.

Mgullu (1990) katika *The Structure of Kiswahili Sentences: A Transformational Generative Approach* ameshughulikia sentensi za lugha ya Kiswahili Kazi hii imetufunulia mengi kuhusu virai mbalimbali vinavyounda vishazi huru. Uchanganuzi wake wa kutenga vitenzi na viambishi vya njeo na upatanishi umetufaa katika kuchanganua viambajengo vya M katika kishazi huru cha Kiswahili Sanifu.

Sewangi (1993) Katika *The Syntax of Empty Category in Kiswahili Simple Sentences: The Government and Binding Approach* amechanganua Kategoria tupu katika sentensi sahili ya Kiswahili. Kazi hii imetufaa kwani ametumia nadharia ya *X-bar* ambayo tumetumia katika kazi yetu.

Hakujibinwa!

Matu (1991) katika kazi yake ya *WH-Movement in Kiswahili* amekuwa na mchango mkuu kwetu. Katika uchanganuzi wake ameitumia nadharia ya *X-bar* kama ambavyo tumeanya. Tofauti iliyopo baina ya kazi yake na yetu ni kuwa yeye amejikita katika sentensi zenyenye maswali na vilevile kazi yake haijashughulikia miundo ya virai vinavyounda vishazi huru.

Wesana-chomi (1973) katika makala ya *Uchambuzi wa Sentensi za Kiswahili* ametusaidia kwa upande wa dhana ya Kishazi huru katika uchanganuzi wake wa sentensi changamano.

Mgullu (1999) katika *Mtalaa wa Isimu-Fonetiki, Fonolojia na Mosolojia ya Kiswahili* ametupa mchango mkubwa kwa kuonyesha upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia kigezo cha kisintaksia ambacho hutumika katika nadharia ya Umilikifu na Masharti

Mgullu *Sintaksia- Utangulizi* (Mswada ambao haujachapishwa) ameeleza kuhusu dhana ya virai na vishazi pamoja na miundo yake japo nadharia aliyotumia si ile ya *X-bar*. Vilevile ameelezea mengi kuhusu kategoria za kiuamilifu katika lugha ya Kiswahili.

Kazi za aina ya pili ni zile zinazohusiana na nadharia ya *X-bar*. Kazi za Radford (1988), *Transformational Grammar* na (1997), *Syntax- A Minimalist Introduction* ndizo kazi mahsusini tulizotumia katika utafiti wetu kama msingi wa kinadharia. Kazi hizi zimetufaa kwani zimetufunulia mengi kuhusu nadharia ya *X-bar* kwa njia sahili zaidi na hasa muundo wa kishazi huru. Japo kazi hizi zimejikita katika lugha ya Kiingereza kuna

mengi ambayo yanaingiliana na yale ya lugha ya Kiswahili. Mbali na hayo kazi hizi zimetupa mwangaza kuhusu malengo ya Sarufi Bia ambayo huongoza nadharia hii ya *X-bar*.

Horrocks (1987) katika *Generative Grammar* ni kazi muhimu kwetu kwa kutupa historia kuhusu maendeleo ya Sarufi Zalishi kutoka nyakati za SGMZ hadi wakati wa nadharia ya UM ambao unahusika na nadharia ya *X-bar*. Kazi hii imetueleza kuhusu nadharia zote zinazounda nadharia ya UM na majukumu yao katika sarufi ya lugha.

Chomsky (1965) katika *Aspects of the Theory of Syntax* ni kazi muhimu kwa kutoa msingi kuhusu muundo wa sarufi ya lugha hasa kile kitengo cha msingi. Welewa wa kitengo hiki umetuwezesha kuelewa zaidi mageuzi yaliyofanyiwa kitengo hiki katika nadharia ya UM

Ouhalia (1991) katika *Functinal Categories and Parametric Variation* ametufaa zaidi katika uchanganuzi wa nadharia ya *X-bar* hasa katika kiambajengo cha M ambapo ametuonesha kwamba kiambajengo hiki huchukuliwa na viambishi vya njeo, upatanishi, yambwa na ukusho. Anaendelea kuonyesha kwamba mpangilio wa viambishi hivi katika kiambajengo hiki cha M hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Kazi hii yake imekuwa muhimu zaidi kwetu Katika utafiti wetu tumeonesha aina zote za viambishi vinavyochukuliwa na kiambajengo hiki.

Vitale (1991) katika *Swahili Syntax* ametufunulia mengi kuhusiana na viambishi vya Kitengo cha M ambavyo vinawakilisha ngeli, virejeshi, njeo, ukusho, na yambwa. Katika kazi yake ameeleza viambishi vyote vya awali katika vitenzi. Ameeleza pia kuhusu viambishi vinavyowekewa nomino na ambavyo vinahusika katika uanishaji

wa nomino katika ngeli mbalimbali na vile ambavyo vinawekewa nomino ili kuunda vielezi hasa vyatia mahali.

Katika uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili Vitale ametupa mwangaza mkubwa kuhusiana na miundo ya sentensi katika umbo lake la ndani na lile zalika. Miundo hii ilitusaidia katika kuelewa zaidi miundo zalika ya vishazi huru japo hatukutumia miundo ya ndani katika utafiti wetu.

Haegeman(1991) katika *Introduction to Government and Binding Theory* ameeleza kwa undani nadharia ya Umilikifu na Masharti ambamo nadharia hii ya *X-bar* imejikita. Katika maelezo yake ya nadharia hizi ametumia mifano kutoka lugha kama vile Kihispaniola na Kiitaliano. Baadhi ya mifano kutoka lugha ya Kiitaliano inaingiliana na ile ya lugha ya Kiswahili hasa kuhusiana na kigezo cha kuachwa kwa kiima katika vishazi pale ambapo viambishi vinavyowakilisha kiima vinavyoambishwa kwenye vitenzi.

Katika kuelezea nadharia ya *X-bar*, Haegeman ameeleza kuhusiana na uchanganuzi wa virai kwa kuzingatia kategoria za kisarufi na vile vile uchanganuzi wa vishazi kwa kuzingatia kategoria za kisarufi na za kiuamilifu. Kazi hii yake imetufunulia mengi ambayo yametusaidia katika kuchunguza muundo wa kishazi huru arifu cha Kiswahili.

## **1.9 NJIA ZA UTAFITI**

Utafiti wetu umekuwa wa maktabani ambapo udurusu wa kazi mbalimbali umefanywa. Utafiti wetu umeendeshwa kwa kutoa mifano ya vishazi huru nya Kiswahili sanifu kutoka kwa lugha ya kimaongezi ambapo tumetumia utaalamu wetu wa lugha ya Kiswahili kuunda vishazi huru mbalimbali. Utafiti wetu pia umeendeshwa kwa kupata ushauri wa kitaalamu kutoka wahadhiri na wasemaji wa lugha ya Kiswahili pamoja na ujuzi wa mtafiti katika lugha ya Kiswahili.

# SURA YA PILI

## 2.1 KATEGORIA

Maneno huainishwa katika kategoria. Kategoria ni kundi la maneno liio na sifa fulani. Maneno huwekwa katika kategoria za aina mbili. Kuna kategoria za kileksika na kategoria za kiuamilifu. Kategoria za kileksika huhusisha maneno ambayo huunda kamusi ya lugha na huonyesha jinsi neno fulani hufanya kazi katika sarufi ya lugha. Kategoria hizi huhusisha aina za maneno kama vile: vitenzi, nomino, vielezi na vihusishi. Kategoria hizi zinaweza kuwa maneno, virai au vishazi. Kategoria za kileksika zinazohusika katika utafiti wetu unahusu virai.

Kategoria za kiuamilifu ni vipashio ambavyo huhusika na ufasiri wa makala na huonyesha jukumu la kipashio fulani katika muundo fulani. Yaani zinafasiri miundo ya kisarufi kwa kuhusisha na mfumo mzima wa lugha. Vipashio hivi huweza kuwa mofu, neno au mafungu ya maneno na hutekeleza majukumu fulani ya kisarufi. Kategoria hii huhusisha vipashio kama vile: kiima, kiarifu, kijalizo, yambwa, kijalizi, vipatanishi, njeo na vibainishi. Pia huhusisha kategoria ambazo ni mvurumisho wa kichwa fulani cha kiuamilifu kwa mfano p-bar na J-bar.

## 2.2 VIRAI

Kirai ni mofu, neno au fungu la maneno ambalo huwakilisha maana fulani katika mfumo mzima wa vishazi. Massamba na wengine (1999) wanasema kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini hakina muundo wa kiima na kiarifu. Awali virai vilihusishwa na mafungu ya maneno lakini maendeleo ya kinadharia yamefanya vipashio kama vile mofu na maneno kuainishwa kama virai. Virai huundwa kutokana na kategoria za maneno na mahusiano maalum baina yao.

Virai lazima viwe na neno moja ambalo ndilo kichwa na ambalo hutawala maneno mengine yanayohusiana nayo. Kichwa hiki hutokana na kategoria za maneno. Kichwa hiki chawea kuwa mwanzoni ama mwishoni kikifuatwa na kijalizo kwa kutegemea lugha husika. Kiswahili huwa muundo wa kirai ambacho hutanguliwa na kichwa na kufuatwa na kijalizo. Uundaji wa virai hujikita katika kategoria za kileksika na kategoria za kiuamilifu.

## 2.2.1 VIRAI VYA KILEKSIKA

Kiswahili kina virai vya kileksika vifuatavyo:

- (i) virai nomino
- (ii) virai vumishi
- (iii) virai elezi
- (iv) virai tenzi
- (v) virai husishi

### 2.2.1.1 Virai Nomino

Nomino ni neno linalotaja kitu, kiumbe, hali, dhana au tendo lolote liwalo. Yaani jukumu lake ni kukipambanua kitajwa. Nomino katika lugha ya Kiswahili huainishwa katika ngeli mbalimbali. Virai nomino huweza kutumika kama kiima au yambwa katika kishazi. Miundo ya virai nomino imejikita kwenye nomino au mahusiano maalum baina ya nomino na neno au mafungu ya maneno. Virai hivi vinatawaliwa na nomino au viwakilishi vyake ambavyo ndivyo vichwa vyake. Virai nomino vya kiswahili huundwa kwa njia zifuatazo:

- (i) Nomino au Kiwakilishi pekee

Kwa mfano:

-Juma alienda sokoni kununua machungwa.

-Mimi ninasoma hapa na wewe pale.

Katika vishazi hivi virai nomino vimepigwa mstari. Miundo ya virai hivi utakuwa:

KN



KN



## (ii) Nomino na kivumishi

Kwa mfano:

-Mtoto wetu amekuja kutoka Mombasa.


-Kaka yangu ni mwalimu

Miundo wa virai hivi utakuwa:

KN



KN




## (iii) Nomino + Kivumishi+ Kielezi

Kwa mfano:

-Mwanafunzi mzuri sana ametuzwa zawadi baada ya kufaulu mtihani wake.

-Kitabu kikubwa zaidi ni kile pale na hiki ni kidogo sana.

Kirai hiki kina muundo ufuatao:




(iv) Nomino + Kivumishi + Kivumishi

Kwa mfano:

-Mtoto wetu mdogo ni mgonjwa.

-Kalamu yangu nyekundu ilipotea jana asubuhi.

Kirai hiki kina muundo ufuatao:




(v) Kibainishi + Nomino

Kwa mfano:

-Hii kazi yangu nitaimaliza sasa hivi.

-Huvu msichana anapenda kusoma sana

Kirai hiki kina muundo ufuatao




(vi) Kibainishi + Nomino + Kivumishi + Kielezi

Kwa mfano:

-Hiki kitabu kizuri sana kimependwa na watu wengi.

-Huvu mtoto mdogo sana anapenda kulialia bila sababu.

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:



## 2.2.1.2 Virai Vumishi

Kivumishi ni aina ya neno ambalo hutoa taarifa zaidi juu ya nomino. Virai vumishi ni virai ambavyo neno kuu ni kivumishi. Virai vumishi huundwa kwa njia zifuatazo.


### (i) Kivumishi + Kivumishi

Kwa mfano:

-Mtoto amevalia nguo fupi nyekundu

-Alinunua viatu vidogo vyeusi vya shule.

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:




### (ii) Kivumishi + Kielezi

Kwa mfano:

-Kiti hicho chako ni kidogo sana.

-Kamba yangu ilikuwa ndefu zaidi

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:



### (iii) Kivumishi + Kivumishi + Kielezi

Kwa mfano:

-Baba alinunua kalamu nyeusi nzuri sana

-Alituzwa zawadi nvingi bora kabisa

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:




(iv) Kivumishi + Kirai elezi

Kwa mfano:

-Kama alinunuliwa viatu vibaya sana sana.

-Sherehe hiyo ya arusı ilikuwa na chakula kingi tele tele.

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:



(v) Kivumishi pekee

Kwa mfano:

Juma ni mzuri

-Vitabu vyake ni viwili

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:

KV  
↓  
mzuni

KV  
↓  
vivili

### 2.2.1.3 Virai Elezi

Kielezi ni neno linalofafanua kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Virai elezi ni virai ambavyo vichwa vyao ni vielezi. Kuna aina kadha za virai elezi katika lugha ya Kiswahili. Virai hivi ni:

- (i) Virai elezi vya wakati
- (ii) Virai elezi vya namna
- (iii) Virai elezi vya mahali
- (iv) Virai elezi viulizi
- (v) Virai elezi vya kiasi


#### 2.2.1.3.1 Virai elezi vya namna

Virai elezi vya namna ni virai ambavyo huwa na vielezi vinavyoeleza jinsi tendo lilivyofanyika.

Kwa mfano:

- Juma alitembea haraka lakini Jane alitembea polepole.
- Juma alianguka vibava sana sana uwanjani.

Kirai hiki huwa na muundo ufuatao:



### 2.2.3.1.2 Virai elezi vyakati


Virai elezi vyakati ni virai ambavyo huwa na vielezi vinavyoeleza wakati tendo lilipofanyika.

Kwa mfano:

-Juma atasafiri kesho kwenda shulenii.

-Tulifika jana usiku sana kutoka safarini.

Kirai hiki huwa na muundo ufuatao:



### 2.2.3.1.3 Virai elezi vyakati


Virai elezi vyakati ni virai ambavyo huwa na vielezi ambavyo vinatoa taarifa kuhusu mahali tendo lilipofanyika.

Kwa mfano:

-Mama anaenda sokoni leo kununua matunda.

-Paka aliingia mumo humo shimonii.

Kirai hiki huwa na muundo ufuatao:



#### 2.2.3.1.4 Virai elezi viulizi


Virai elezi viulizi huwa na vielezi ambavyo huuliza maswali kuhusiana na matendo au hali mbalimbali.

Kwa mfano:

-Juma alienda wapi?

-Unafanya nini?

Kirai hiki kina muundo ufuatao:



### 2.2.3.1.5 Virai elezi vyakiasi

Virai elezi vyakiasi huwa na velezi vinavyoonyesha kiasi cha matendo au hali.

Kwa mfano:

Baba alichoka sana.

Mimi nimeshiba zaidi.

Kirai hiki kina muundo ufuatao:



### 2.2.4 Virai tenzi

Kitenzi kulingana na Kihore na wengine (2001:131) ni aina ya meno ambalo linatoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalitendwa na kiumbe au kitu. Kirai tenzi ni meno ama fungu la maneno ambalo huwa na kitenzi kama kichwa cha kirai. Kirai tenzi huambishwa viambishi awali vyakiasi cha mnyambuliko na viambishi tamati vyakiasi kauli na dhamira. Katika utafiti wetu tumeangalia viambishi awali pekee. Kirai tenzi huweza kuwa pekee au kikifuatwa na kijalizo hasa katika vitenzi vishirikishi virai elezi ama virai husishi. Kiswahili kina aina tatu za vitenzi hivyo tunaweza kuwa na virai vilivyo na aina hizi za vitenzi vikiwa vichwa:

-virai tenzi vishirikishi

-virai tenzi visaidizi

-virai tenzi vikuu

Virai tenzi vishirikishi ni virai ambavyo huhitaji vijalizo ili viwe kamilifu. Virai hivi huhitaji vijalizo ambavyo vinaweza kuwa nomino, kielezi au kivumishi. Virai tenzi hivi haviambishwi mofu za njeo kwani njeo huchukuliwa kuwa wakari uliopo lakini huambishwa mofu za upatanishi.


Kwa mfano:

-Yeye ni mwalimu

-Mtoto yuko nyumbani

-Karisa ana kalamu

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:



Virai tenzi visaidizi ni vitenzi ambavyo vinaandamana na vitenzi vikuu hasa pale ambapo vitenzi husika vinahusisha hali. Katika hali hii kitenzi kisaidizi huchopekwa kabla ya kitenzi kikuu na kuambishwa mofu za upatanishi na njeo ili kuonyesha njeo huku kitenzi kikuu kikiambishwa mofu za upatanisho na hali ili kuonyesha hali.


Kirai hiki hivyo basi huhusisha vitenzi viwili na kufuatwa na virai nomino, virai elezi au virai husishi.

Kwa mfano:

-Jane alikuwa anaenda dukani.

Alikuwa amechelewa kufika.

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:





Vitenzi vikuu ni vitenzi ambavyo vimeambishwa mofu za viambishi awali vyamnyambuliko katika vitenzi. Vitenzi hivi hubeba maana kuu ya kitenzi na hujitokeza vikiwa pekee au vikifuatwa na virai elezi, virai nomino na virai husishi.

Kwa mfano:

- Mama analima shamba
- Kitabu kimeanguka
- Jane ameenda shulen
- Paka analala katika nvumba.

Kirai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:



## 2.2.5 Virai husishi


Vihusishi ni maneno yanayounganisha mahusiano baina ya vitenzi kwa upande mmoja na virai nomino katika upande wa pili ili kupata kishazi kimoja. Virai husishi ni virai ambavyo vichwa vyao ni vihusishi. Virai husishi mara nyingi huwa na kihuishi kinachofuatwa na kirai husishi kingine au kirai nomino.

Kwa mfano:

- amepigwa kwa fimbo
- Juma amesafiri hadi Mombasa.

-Juma anaketi na babake.

Krai hiki kitakuwa na muundo ufuatao:



## 2.3 KATEGORIA ZA KIUAMILIFU

Kategoria za kiuamilifu ni aina ya maneno yasiyo na maana ya kileksika bali iliyo na maana ya kisarufi. Hurejelea kategoria ambazo hutekeleza majukumu fulani ya kisarufi katika tungo. Katika utafiti wetu tumeangalia kategoria zifuatazo za kiuamilifu:

- (i) Kiima
- (ii) Kiarifu
- (iii) Chagizo
- (iv) Kijalizo
- (v) Yambwa
- (vi) Kibainishi
- (vii) Kijalizi
- (viii) Njeo
- (ix) Kipatanishi

### 2.3.1 KIIMA

Kulingana na kamusi ya TUKI (1990) kiima ni kipashio ambacho huelezwa na kiarifu. Kiima hutawala umbo la kishazi kwa kuwa na vipatanishi ambavyo vinajitokeza kama viambishi katika maneno mengine katika tungo husika. Kiswahili kama lugha

inayoweza kuacha kuonyesha kiima huwa na vipatanishi vinavyotambulisha kiima cha kishazi. Kiima mara nyingi huwa ni virai nomino au viwakilishi vyake. Kiima katika lugha ya Kiswahili huwekwa katika makundi yanayoitwa ngeli. Katika jedwali lifuatalo kichwa cha kirai kinachochukua nafasi ya kiima hutawala upatanisho baina ya kichwa hicho na maneno mengine katika kishazi.

KIIMA	VIPATANISHI
Mtoto mzuri	m
Watoto wazuri	wa
Kiti hiki kizuri	ki,ki
Vitabu hivi vizuri	vi,vi
Huyu msichana mrefu mrembo	yu, m,m
Hawa wasichana warefu warembo	wa, wa wa
Mti huu ulio mfupi	u, u, m
Kelele hizo zao	zo, z-
Macho haya yangu	ya, ya

### 2.3.2 KIARIFU

Kiarifu hueleza tendo linalohusika katika tungo. Kimsingi viarifu huwa ni virai tenzi ambavyo vimeambishwa mofu za mnyambuliko, vya dhamira na vya kauli. Mizizi ya viarifu katika tungo zifuatazo zimeandikwa katika herufi nzito.

Kwa mfano:

-Juma a-na-li-a

-Mwalimu a-na-som-esh-a

-Baba ni daktari.

### **2.3.3 YAMBWA**

Yambwa ni aina ya neno ambalo huashiria anayetendewa jambo fulani ama kile ambacho kinapokea kitendo. Aghalabu yambwa tendwa na tendewa huwa ni nomino au virai nomino. Yambwa tendwa ni ile ambayo inapokea tendo moja kwa moja ilhali yambwa tendewa ni ile inayotendewa jambo fulani. Katika kishazi kilicho na yambwa tendewa yambwa tendwa ni lazima iwepo na hujitokeza baada ya yambwa tendewa. Lughya ya Kiswahili huambisha vipatanishi vya yambwa kwenye virai tenzi kabla ya mzizi wa kitenzi na vipatanishi hivi huwa vya yambwa tendewa pale ambapo yambwa tendewa kipo kwenye kishazi. Vipatanishi hivi huwa vipatanishi vya nafsi na vya ngeli.

Kwa mfano:

-Mama alimbeba mtoto.

Yambwa tendwa hapa ni mtoto na kiambishi kilichoandikwa kwaa herufi nzito ndicho kipatanishi chake.

-Kaka alimpikia miomba chakula.

Yambwa tendewa hapa ni mjomba na chakula ni yambwa tendwa. Kiambishi kilichoandikwa kwa herufi nzito ni kipatanishi cha yambwa tendewa.

### **2.3.4 KIBAINISHI**

Istilahi hii hutumika kwa maana mbili. Kibainishi ni kipashio kinachodhiihirisha kwa ufasaha zaidi urejeleo wa nomino. Mara nyingi vionyeshi vinapotangulia kiuma huwa ni vibainishi. Mbali na nomino tumetumia istilahi hii kurejelea kategoria nyingine ambayo inadhihirisha kwa ufasaha zaidi urejeleo wa kategoria fulani mahsus. Vichwa vya virai huwa na upatanisho na vibainishi vyake. Upatanisho huu huwa wa idadi, ngeli na nafsi. Kategoria inaweza kuwa au kutokuwa na kibainishi hivyo nafasi hii inaweza kuwa imejazwa au kuwa kapa. Katika muundo wa kishazi kibainishi KB huchukuliwa na kira

nomino KN ambacho ni kiuma cha kishazi. Aidha katika muundo wa kirai tenzi KT, kitenzi kisaidizi Ts huchukua nafasi ya kibainishi KB.

Kwa miano:

- Huyu mwanangu ni mgonjwa.
- Kile kitabu chake kimepotea.
- Jane alikuwa akienda Mombasa.

### 2.3.5 KIJALIZI

Hi ni kategoria nyingine ya kiuamilifu na hutumika kutanguliza vishazi. Katika Kiswahili vijalizi ni maneno kama vile: kama , ikiwa, kwa sababu, ingawa, kuwa, baada ya , mpaka na kadhalika.Katika vishazi huru nafasi hii ya kijalizi huwa tupu lakini katika vishazi tegemezi nafasi ya vijalizi huwa imejazwa. Katika vishazi vijalizi hutumika kama ifuatavyo:

- ØJuma alisema kuwa *ataenda shulen*.
- ØMwizi alishikwa kwa *kipattikana na hatia ya wizi*.
- ØAlikuja ingawa *aliarwa amechelewa*.

Katika vishazi hivi vishazi tegemezi vimeandikwa kwa herufi za mlazo na vijalizi vimeonyeshwa kwa herufi nzito. Katika kishazi huru nafasi hii ni tupu hivyo kinawakilishwa na mofu kapa.

### 2.3.6 KIAMBAJENGO CHA MNYAMBULIKO (M)

Kiambajengo hiki cha M huonyesha nafasi ambayo awali ilichukuliwa kuwa kategoria moja na ambayo baadaye ilivunjwa katika vipengele mbalimbali. Kiambajengo hiki hurejelea nafasi za viambishi awali vya vitenzi. Vipengele hivi ni viambishi vya njeo (n), vipatanishi (p), ukanusho (o), hali (l) na yambwa (y). Viambishi hivi hutekeleza majukumu maalum ya kisarufi . Kulingana na nadharia tete ya kukivunja kirai hiki (*Split*

*INFL Hypothesis), kila mojawapo wa viambishi hivi huchukuliwa kuwa kirai kinachojisimamia na kinachotawala mvurumisho wake.*

Kutokana na nadharia hii hivyo basi, viambishi hivi huwa virai vyenye vichwa mbalimbali yaani kirai kipatanishi (Kp), kirai njeo(Kn) kirai kanusho (Ko), kirai hali (Kh) na kirai yambwa (Ky). Katika utafiti wetu tumeangalia virai vipatanishi (Kp), virai njeo (Kn) na virai yambwa (Ky).

### **2.3.6.1 KIRAI KIPATANISHI (Kp)**

Kirai kipatanishi hujitokeza mwanzoni mwa viambishi vyta mnyambuliko katika vishazi yakinishi na na inaweza tu kutanguliwa na kirai cha ukusho katika vishazi kanushi.

Kiswahili kina aina mbili za vipatanishi:

- vipatanishi vyta nafsi
- vipatanishi vyta ngeli.

Vipatanishi vyta nafsi huanishwa kwa kuzingatia nafsi. Kuna nafsi za aina tatu katika Kiswahili na ambazo zinatumika hasa katika ngeli ya kwanza yaani M-Wa. Hata hivyo nafsi ya tatu hutumika kurejelea nomino za ngeli zile zingine. Nafsi hizo pamoja na viambishi vyake ni kama ifuatavyo:

<u>NAFSI</u>		<u>VIAMBISHI</u>	
Umoja	Wingi	Umoja	Wingi
1. Mimi	Sisi	ni-	tu-
2. Wewe	Nyinyi	u-	m-
3. Yeye	Wao	a-	wa-

Kwa mfano:

<u>UMOJA</u>	<u>WINGI</u>
-Mimi ninaenda	-Sisi tunaenda
-Wewe unaimba	-Nyinyi mnaimba
-Yeye anacheka	-Wao wanacheka

Vipatanishi vya ngeli huainishwa kwa kurejelea upatanisho baina ya nomino na maneno mengine hasa vitenzi. Vipatanishi hivi hutumika katika uainishaji wa nomino za kisintaksia. Vipatanishi hivi huwa ni hivi vifuatavyo:

## A-WA

Vipatanishi hivi hutumika kwa nomino zenyе kutaja viumbe. Kipatanishi A- hutumika katika umoja na kipatanishi Wa- katika wingi. Vipatanishi hivi hutumika katika ngeli ya M-Wa ambayo huainishwa kwa kuzingatia viambishi awali vya nomino husika. Mifano ya nomino zenyе kutumia vipatanishi hivi ni kama vile: mtu, simba, kijana, kuku, mtoto, shangazi na mnyama. Vipatanishi hivi hutumika kama ifuatavyo katika vishazi huru:

<u>UMOJA</u>	<u>WINGI</u>
-Mama anapika chakula.	-Akina mama walipika vyakula.
-Kuku alichinjwa jana.	-Kuku walichinjwa jana.
-Mtoto analia sana.	-Watoto wanalia sana.

## U-I

Vipatanishi hivi hutumika kwa nomino zinazohusisha majina ya miti na mimea . Sehemu za mwili na vifaa mbalimbali. Kipatanishi U-hutumika katika umoja na I- katika wingi. Vipatanishi hivi hutumika kwa nomino za kimofolojia za M-Mi. Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni kama vile: mkono, mti, mwiko, mchungwa na mguu. Vipatanishi hutumika kama ifuatavyo katika vishazi huru:

<u>UMOJA</u>	<u>WINGI</u>
--------------	--------------

-Mti umeanguka

-Miti imeanguka

-Mkono wangu unauma.

-Mikono yangu inauma.

-Mkuki ulirushwa mbali

-Mikuki ilirushwa mbali

## LI-YA

Vipatanishi hivi humika kwa nomino ambazo huchukua kiambishi Ji-, J au mofu kapa katika umoja na Ma- katika wingi. Baadhi ya nomino zenyе kutumia vipatanishi hivi ni kama vile: jino, jembe, embe, gari, zulia na jaa. Vipatanishi hivi hutumika kama ifuatavyo katika vishazi huru:

### UMOJA

-Jembe limenunuliwa

### WINGI

-Majembe yamenunuliwa.

-Chungwa limeanguka

-Machungwa yameanguka.

-Gari letu liliharibika.

-Magari yetu yaliharibika.

## KI-VI

Vipatanishi hivi hutumika kwa nomino zenyе viambishi Ki- au Ch- katika umoja na Vi- au Vy- katika wingi. Baadhi ya nomino zenyе kutumia vipatanishi hivi ni kama vile: kitu, chakula, cheti, kisu, kikombe na chama. Vipatanishi hivi hutumika katika vishazi huru kama ifuatavyo:

### UMOJA

-Kiti kimevunjika.

### WINGI

-Viti vimevunjika.

-Chama cha kimeundwa.

-Vyama vyao vimeundwa.

-Kisu kikali kilinunuliwa.

-Visu vikalii vilinunuliwa.

## I-ZI

Vipatanishi hivi hutumika kwa nomino zenyе viambishi tofauti tofauti. Baadhi ya nomino zenyе kutumia viambishi hivi ni kama vile: ndoo, ndizi sabuni, pesa na kamba.

Vipatanishi hivi hutumika kwenye vishazi huru kama ifuatavyo:

### UMOJA

- Kalamu yangu imepotea.
- Ndizi imenunuliwa.
- Sabuni imeisha.

### WINGI

- Kalamu zetu zimepotea.
- Ndizi zimenunuliwa.
- Sabuni zimeisha.

## U-ZI

Vipatanishi hivi hutumika kwa nomino zenyе viambishi U- ama W- katika umoja na M-, N-, Ny- ama mofimu kapa katika wingi. Baadhi ya nomino zenyе kutumia viambishi hivi ni kama vile: uso, ubao, wembe, uzi na ua. Vipatanishi hivi hutumika kama ifuatavyo kwenye vishazi huru:

### UMOJA

- Uso wake unapendeza.
- Ua ulijengwa kwangu.
- Ubao umefutwa.

### WINGI

- Nyuso zao zinapendeza.
- Nyua zilijengwa kwetu.
- Mbao zimefutwa.

## U-YA

Vipatanishi hivi hutumika kwa nomino zenyе kuchukua viambishi awali U- katika umoja na Ma- katika wingi. Baadhi ya nomino zenyе kutumia viambishi hivi ni kama vile: ugonjwa, umbo, uovu na ugomvi.

Vipatanishi hivi hutumika kama ifuatavyo kwenye vishazi huru:

### UMOJA

- Ugonjwa huo umetibiwa.
- Uovu unachukiza.
- Ugomvi wao umeisha.

### WINGI

- Magonjwa hayo yametibiwa.
- Maovu yanachukiza.
- Magomvi yao yameisha.

## **U**

Kipatanishi hiki hutumika kwa nomino zisizoweza kuhesabika. Baadhi ya nomino zinazotumia kipatanishi hiki ni kama vile: umande, utoto, ulevi, uzuri na usingizi.

Kipatanishi hiki hutumika kama ifuatavyo kwenye vishazi huru:

- Uzuri wake uliwapendeza.

- Usingizi umenipalia.

- Ulevi wake unamwathiri.

## **YA-**

Kipatanishi hiki hutumika kwa nomino zinazopatikana katika hali ya wingi tu. Baadhi ya nomino zenyе kutumia kipatanishi hiki ni kama vile; maji, maziwa, manukato na mate.

Kipatanishi hiki hutumika kama ifuatavyo kwenye vishazi huru:

- Maziwa yamenunuliwa.

- Manukato hayo yanapendeza.

- Maji yameisha.

## **I-**

Kipatanishi hiki hutumika kwa nomino zinazotaja vitu kwa ujumla. Baadhi ya nomino zenyе kutumia kipatanishi hiki ni kama vile: sukari, chumvi, chai, sumu na pombe.

Kipatanishi hiki hutumika kama ifuatavyo kwenye vishazi huru:

- Sukari imeisha.

- Chumvi imemwagika.

- Pombe imenunuliwa.

## **KU**

Kipatanishi hiki hutumika kwa vitenzi vilivyonominishwa. Nomino hizi hayana <sup>hezina</sup> umoja wala wingi. Baadhi ya nomino zenyе kutumia kiambishi hiki ni kama vile: kusoma kulia, kwenda, kupika na kuchora. Kipatanishi hiki hutumika kama ifutavyo kwenye vishazi huru:

-Kusoma kwake kunapendezza.

-Kupika huko kunavutia.

-Kwenda kwao kilitufurahisha.

## PA-KU-MU.

Vipatanishi hivi hutumika kwa nomino zenyе kuaashiria mahali. Kipatanishi Pa-hutumika kurejelea mahali maalum, Kipatanishi Ku- kurejelea mahali kusiko maalum na kipatanishi Mu-kurejelea mahali ndani. Vipatanishi hivi hutumika kama ifuatavyo kwenye vishazi huru:

-Mahali hapo panatakikana.

-Mahali huko kunatakikana.

-Mahali humo mnatakikana.

### 2.3.6.2 KIRAI CHA YAMBWA (Ky)

Kirai cha yambwa huonyesha upatanisho wa yambwa na huambishwa karibu na kitenzi baada ya kiambishi cha kirai njeo. Kiambishi hiki hutumia vipatanishi kama vile vya kiima kwa kutegemea ngeli ya yambwa husika. Mbali na hivyo kuna vipatanishi vinavyowakilisha nafsi ya yambwa katika ngeli ya M-Wa. Vipatanishi hivi ni:

<u>Nafsi</u>	<u>Kipatanishi</u>	
Mimi-Sisi	ni-	tu-
Wewe-Nyinyi	ku-	wa-
Yeye-Wao	m-	wa-
Ngeli, Ji-Ma	li-	ya-

Vipatanishi hivi hutumika kama ifuatavyo kwenye vishazi huru:

## UMOJA

-Mama aliniletea kitabu

## WINGI

-Vijana walituletea vitabu


- Kitabu kilikupendeza. -Vitabu viliwapendeza
- Kaka alimwambia hivyo. -Akina kaka waliwaambia hivyo.
- Kamau aliukata mti. -Akina kamau waliikata mti.
- Alilinunua gari hilo. -Waliyanunua magari hayo.

Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha upatanisho baina ya kiima (ngeli), vipatanishi nya ngeli, idadi na nafsi pamoja na vipatanishi nya yambwa na matumizi yake katika vishazi.

Katika jedwali hili tumetumia nambari kuwakilisha ngeli mbalimbali


GELI	VIPATANISHI	YAMBWA	MIFANO
1	ni tu	ni tu	Mimi nilisema/Sisi tulisema/Alinipiga/Alitupiga
	u m	ku wa	Wewe ulinisema/Nyinyi mlitusema/Alikuacha/mliwasema
	a wa	m wa	Yeye alikupiga/Wao waliwapiga/Ninampiga/Tunawapiga
4	u i	u i	Mti ulikatwa /Miti ilikatwa/Aliukata/Aliikata
5	li ya	li ya	Jino linauma/Meno yanauma/Aliling' oa/Waliyang' oa
8	ki vi	ki vi	Kiti kinafaa/Viti vinafaa/Ulikinunua/Mlivununua
10	I zi	i zi	Ndoo imeshwa/Ndoo zimeoshwa/Umeileta/Mmezileta
11-12	u zi	u zi	Uzi umekatwa/Nyuzi zimekatwa/Ameukata/Wamezikata
13-14	u ya	u ya	Uovu umeneea/Maovu yameenea/Anaulipa/Mnayalipa
15	ya	ya	Maji yameisha /Ameyanywa/Wameyanywa
16	u	u	Uzuri unafaa/Aliupenda/Waliupenda
17	i	i	Chai imejaa/Ameipika/Wameipika
18	ku	ku	Kusoma kunachosha/Anakupenda/Wanakupenda
19-21	pa ku mu	pa ku mu	Mahali panafaa/kunafaa/mnafaa/ Anapapenda/Anakupenda/ Wanamokaa

Kutokana na haya muundo wa kiambajengo M utakuwa



Mfano wa muundo wa kishazi:

-Mtoto anasoma kitabu



## SURA YA TATU

### 3.1 MUUNDO WA KISHAZI HURU

Mathews (1997) katika *A Concise Dictionary of Linguistics* anasema kuwa kishazi ni kipashio chochote cha kisintaksia ambacho umbo lake limeshuswa au kuonekana kushushwa daraja kutoka ile ya sentensi. Aghalabu huhusisha kitenzi na elementi zingine zinazoandamana nacho. Radford (1997) anasema kuwa kishazi ni kipashio kilicho na kiima na kiarifu na ambacho kinaweza kuhusisha vipashio vingine kama vile vijalizo na chagizo. Mara nyingi kiarifu cha kishazi huwa si kisaidizi bali ni kitenzi cha kileksika. Vishazi hivyo basi ni vipashio vyatya kumuundo ambavyo vipti ya sentensi na virai. Vishazi ni vidogo kuliko sentensi na kubwa kuliko virai. Vishazi huwa na muundo wa kiima na kiarifu hivyo kuwa sawa kabisa kumuundo na sentensi. Tofauti baina ya kishazi ni kwamba kishazi ni <sup>L.P.</sup> ~~kiambajengo~~ cha sentensi ilhalii sentensi si <sup>?</sup> ~~kiambajengo~~ cha kipashio kingine. Vishazi huwa vimeshushwa daraja na hutumika kama viambajengo vyatya sentensi nyingine. Vishazi hivyo basi huweza kuchopekwa ndani ya sentensi zingine. Vishazi vinaweza kuwa huru ama tegemezi. Vishazi huru ni vile ambavyo vinaweza kusimama pekee kama sentensi kamili. Kwa mifano:

- Juma anacheza.
- Mtoto anaenda dukani.
- Watoto wanalala sasa.

Vishazi tegemezi ni vile ambavyo vikiondolewa katika muktadha wa sentensi havivwezi kusimama pekee yaani vimechomekwa ndani ya vishazi huru. Katika mifano ifuatayo, vishazi tegemezi vimepigwa mstari.

- Mtoto alivekuja iana ameondoka.
- Alipoitwa aliitika.

-Alinunuliwa garı lililokuwa likiuzwa.

-Mama alisema kuwa atakuja kesho.

Sentensi sahili vinapotumika kama viambajengo vya sentensi nyingine hugeuka kuwa vishazi huru.

Vishazi huru vitakavyoshughulikiwa ni vile arifu. Vishazi vinaweza kuainishwa kwa kuzingatia vigezo kama vile: dhamira, kauli, uyakinishi, na muundo. Kwa kuzingatia kigezo cha dhamira, vishazi vinaweza kuwa arifu, ulizi, agizi au vya hisi.

Vishazi ulizi huuliza maswali.

Kwa mfano:

-Wewe unaitwa nani?

-Unaenda wapi?

Vishazi agizi huamuru jambo fulani lifanywe. Kwa mfano:

-Niletee maji.

-Tokeni hapa.

-Tafadhali nyamaza.

Vishazi vya hisi hunuia kuonyesha hisia fulani. Kwa mfano:

-Ala! Umeanguka!

-Lo! Ameumia vibaya.

Vishazi arifu ni vile ambavyo hutueleza juu ya jambo fulani. Kwa mfano:


-Jina langu ni Jerono.

-Mtoto anacheza.

-Juma hataenda shulen ieo.

Vishazi huundwa kutokana na mahusiano maalum ya virai mbalimbali. Katika utafiti wetu tumelenga kuonyesha muundo wa kishazi huru cha Kiswahili na muundo wa kirai cha kiswahili kwa mujibu wa nadharia ya *X-bar*. Katika kufanya hivi tumeonyesha sintaksia ya virai kwa mujibu wa nadharia hii ya *X-bar* katika sura ya pili.

Kwa mujibu wa nadharia hii ya *X-bar*, vishazi huundwa kwa kuunganisha virai mbalimbali. Kila kirai kimsingi ina mvurumisho wa kichwa chake katika bar mbili ambapo bar ya pili ni ya juu kabisa na inayowakilisha kirai kamili kama ilivyo katika muundo ufuatao:




Katika muundo huu kibainishi na kijalizo chawea kuwepo ama kuwa kapa.

Katika maelezo yetu ya nadharia ya *X-bar* katika sehemu ya 1.6, vishazi vimeonekana kuwa na miundo iliyo na kijalizi kinachotanguliza kishazi. Kijalizi hiki katika vishazi huru huwa kapa. Mbali na hayo muundo wa kishazi pia umeonekana kuwa na kiambajengo cha M ambacho kimevunja katika vichwa mbalimbali ambavyo kila kinatawala mvurumisho wake. Katika muundo huu kiima cha kishazi huchukua nafasi ya kibainishi cha kirai kipatanishi kwa kuambatana na kaida ya vibainishi. Hivi ni kusema kirai nomino ambacho hakina upatanisho na kirai kipatanishi hakichukui nafasi hii bali huchukua nafasi ya kijalizi.

Vishazi vyaweza kuwa na yambwa tendwa au yambwa tendewa. Kirai cha upatanisho wa yambwa hujitokeza katika nafasi kabla ya kirai tenzi. Kishazi kilicho na yambwa tendewa lazima ihusishe yambwa tendwa na katika hali hii kirai yambwa huwakilisha yambwa tendewa.

Kirai njeo huchukua nafasi baada ya kirai kipatanishi na kirai tenzi huchukua mofu hizi kwa kirai tenzi hiki kusonga hadi kufikia kirai kipatanishi ili kukiwezesha kuchukua viambishi hivi vya mnyambuliko.



Katika sehemu tumeonyesha miundo ya vishazi huru mbalimbali kwa mujibu wa nadharia hii ya *X-bar*.

### 3.1.1 Kishazi huru chenye kitenzi kisoelekezi.



Kitenzi kisoelekezi ni kitenzi ambacho hakichukui yambwa. Katika mifano ifuatayo

- kishazi huru kimepigiwa mstaru

(i) Mtoto anacheza na Juma anasoma.

(ii) Mama anaenda nyumbani kutoka sokoni.

Katika mifano (i) kuna vishazi huru viwili vilivyounganishwa kwa kiunganishi kiambatanishi *na*. Vishazi hivi vina miundo ifuatayo:



Katika vishazi hivi kuna virai nomino vilivyo na nomino pekee yaani, *mama*, *mtoto* na *soko* ambavyo ni virai kamili. Aidha kuna kirai elezi *nyumbani* na kirai husishi *kutoka* ambavyo vyote ni maneno yanayojisimamia kama virai kamili. Vilevile kuna mofu ambazo ni virai kamili yaani;

A-WA

{a} ambacho ni kipatanishi cha nafsi ya tatu katika ngeli ya M-Wa na mofu {na} ya njeo iliyopo.


### 3.1.2 Kishazi huru chenye kitenzi elekezi.


Kitenzi elekezi ni kitenzi ambacho hakiwezi kukamilika kimaana bila ya kuwa na yambwa. Katika mifano ifuatayo vishazi huru vimepigiwa mstari:

(i) Yule baba alimnunulia mwanawewe kitabu ili akisome.

(ii) Kijana mbaya alikitupa kitabu majini na kutoroka.

Katika mfano (i) yambwa tendewa mwanawewe inawakilishwa katika kitenzi na mofu {m} na katika mfano (ii) yambwa tendwa kitabu inawakilishwa katika kitenzi na mofu ya ngeli husika{ki}. Vishazi hivi vina miundo ifuatayo:





Katika mifano (i) hapo juu kuna yambwa tendewa *mwanawe* inayowakilishwa na kiwakilishi chake cha kirai yambwa {m} kwa sababu mwanawewe huwa katika nafsi ya tatu na hicho ndicho kiwakilishi chake. Katika kishazi hiki yambwa tendwa *kitabu* hakiwakilishi<sup>7</sup> katika mnyambuliko wa kitenzi. Vilevile kiima cha kishazi hiki kimeundwa kutokana na kirai nomino kilicho na kibainishi na kirai nomino.

Katika mifano (ii) yambwa tendwa *ni kitabu* na imewakilishwa katika mnyambuliko wa kitenzi na kirai yambwa {ki} ambacho ni kipatanishi cha ngeli ya Ki-Vi. Aidha mifano huu unahuisha kiima kilicho na kirai nomino kinachoundwa kutokana na nomino na kivumishi *kijana* na *mbaya*.

### 3.1.3 Kishazi kisicho na kiima

Kwa mfano:



(i) Tutakapoitwa tutaitika haraka

(ii) Ninaenda shulen ieo mapema sana

Katika mfano (i) kishazi huru kimepigiwa mstari hivi kumaanisha kwamba kishazi huru chawenza kutangulia kishazi tegemezi au kuja baada yake. Katika kishazi hiki kiima *sisi* imeachwa na kiwakilishi chake kuonyeshwa kwa kipatanishi {tu} ya nafsi ya kwanza wingi. Nafasi hii hivyo basi imewakilishwa na kifupisho *pro* cha viwakilishi.

Katika mfano (ii) kiwakilishi kipatanishi ni {ni} cha nafsi ya kwanza umoja na vilevile kiima kilichoachwa kinawakilishwa na kifupisho *pro*. Katika mfano huu kuna kirai elezi kinachofuatwa na kirai elezi kingine yaani *shulen ieo mapema*. Kirai cha kwanza ni cha mahali na kile cha pili ni cha wakati. Virai elezi hutekeleza jukumu la chagizo katika kishazi hiki. Viambishi vya njeo viliviyotumika ni cha wakati ujao {ta} katika mfano (i) na cha wakati uliopo {na} katika mfano (ii).

Vishazi hivi vitakuwa na miundo ifuatayo:



### 3.1.4 Kishazi kilicho na kirai husishi


Kwa mfano:


(i) Kalamu hivo nyeusi itawekwa juu ya kabati ili mtoto asiifiki.

(ii) Mgeni atahutubu kwenye mkutano huo baada ya maombi kufanywa.

Katika mifano hii vishazi huru vimepigiwa mstari na katika mfano (i) kirai husishi kinachohusika katika kishazi hiki ni *ya* na katika mfano (ii) kirai husishi ni *kwenye*. Virai husishi hivi vinafuatwa na virai nomino *kabati* katika mfano (i) na *mkutano huo* katika mfano (ii). katika mfano huo wa (i) kirai nomino ambacho ni kiima cha kishazi kimeundwa kutokana na kirai nomino kilicho na nomino ambacho ni kichwa chake na kirai vumishi kilicho na vivumishi *hiyo* na *nyeusi*. Kiima cha mfano (ii) ni kirai nomino kilicho na nomino pekee.

Vishazi hivi vitakuwa na miundo ifuatayo:





### 3.1.5 Kishazi chenye kitenzi kishirikishi



Kwa mfano:

(i) Grace ana kalamu yangu niliyonunua jana.

(ii) Gari letu liko barabarani likitengenezwa.

Vishazi huru katika mifano hii imepigwiwa mstari. Katika mfano (i) kitenzi kishirikishi ni -na na katika mfano (ii) ni -ko. Vitenzi hivi vimeambishwa mofu za upatanishi {a} ya nafsi ya tatu umoja katika mfano (i) na mofu {li} ya upatanishi wa ngeli ya Ji-Ma katika hali ya umoja. Vitenzi hivi havihusishwi na kiambishi cha njeo hivyo nafasi hii kubakia kapa japo njeo hii huchukuliwa kuwa ule wa wakati ulio[po]. Kitenzi hiki katika mfano (i) hufuatwa na kirai nomino na katika mifano (ii) hufuatwa na kirai elezi.

Vishazi hivi vina miundo ifuatayo:




## Kishazi kilicho na kirai elezi

Kwa mfano:

(i) Mtihani ulikuwa mgumu tena sana sana.

(ii) Wewe ulikimbia mbio sana uwanjani.

Katika mifano hii virai tenzi vinafuatwa na vielezi kadha yaani, katika mfano (i) kuna kirai elezi *mgumu* cha namna, kirai elezi kingine *tena* cha kiasi na kirai elezi kingine *sana sana* cha namna. Katika mfano (ii) kirai elezi *mbio* ni cha namna, kirai elezi *sana* ni cha kiasi na kirai elezi *uwanjani* ni cha mahali. Kirai nomino katika mfano (i) ni cha ngeli ya M-Mi katika umoja na katika mfano (ii) ni kiwakilishi cha nafsi ya pili katika hali ya umoja. Vishazi hivi vina muundo ufuataao




## Kishazi kilicho na kirai vumishi

Kwa mfano:

Sara alinunua nguo mbili ndefu sana na Juma akanunua tatu ndefu zaidi.

Sentensi zilizopigwa mstari ni vishazi huru vilivyounganishwa na kiunganishi kiambatanishi *na*. Katika mfano huu kirai vumishi kimefuatwa na kirai vumishi kingine chenye kivumishi *ndefu* na kielezi *sana*. Kielezi hiki kinaelezea juu ya kivumishi, katika uwakilishi wake vishazi hivi vina muundo sawa.

Vishazi hivi vina muundo ufuatao:



## SURA YA NNE

### 4.1 HITIMISHO

Utafiti wetu umechunguza na kuonyesha jinsi nadharia ya *X-bar* inaweza kutumika kuonyesha miundo ya virai na vishazi huru arifu nya Kiswahili. Katika kufanya hivi utafiti wetu umeonyesha miundo ya virai mbalimbali vikiwemo virai nya kileksika kama vile: virai nomino, vitai tenzi, virai vumishi na virai husishi pamoja na virai nya kiuamilifu kama vile virai vipatanishi, virai njeo, virai yambwa na virai jalizi. Viambajengo vinavyounda virai hivi pia viimeonyeshwa pamoja na mahusiano yao.

Utafiti huu vilevile umeonyesha miundo ya vishazi huru kwa kuzingatia vishazi huru arifu ambazo zinajisimamia pamoja na vile ambavyo vishazi tegemezi huchopekwa ndani yake.

Katika kufanya hivi tumeweza kubainisha kwamba kishazi huru kina kijalizi ambacho hutanguliza vishazi na ambacho katika lugha ya Kiswahili ni kapa. Aidha tumeweza kubainisha kwamba viambishi awali nya mnyambuliko wa kitenzi vinaweza kuchukuliwa kama virai kamili ambavyo kila inatawala mvurumisho wake. Kutokana na haya tumeweza kuonyesha kwamba virai si fungu la maneno pekee bali vinaweza kuwa mofu, maneno yanayojisimamia pekee au mafungu ya maneno.

Utafiti wetu vilevile umebainisha kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo inaweza kuacha kuonyesha kiima katika baadhi ya matumizi yake kutokana na hali yake ya kuwa na viambishi vinavyoweza kutumika kuonyesha kiima yaani (*pro drop language*)

Ingawa hatukuingilia uhamisho wa vipashio mbalimbali katika kishazi huru, kira tenzi cha Kiswahili huhama kutoka mahali pake hadi kufikia kira kipatanishi ili kuweza kujihusisha na viambishi vya mnyambuliko vya upatanishi, njeo au yambwa.

Kwa mujibu wa nadharia tete ambayo tulikuwa tukichunguza tumeweza kuhitimisha kwamba kifungutenzi ambacho hubeba uarifu wa kiima vilevile hubeba kiima cha kishazi kutokana na sababu kuwa kiima cha kitenzi hupata jukumu lake kutokana na kiarifu husika.

Tumeweza vilevile kubainisha kwamba nadharia ya *X-bar* inaweza kutumika katika kuonyesha muundo wa kishazi huru na hivyo kudhihirisha ubia wake.

## 4.2 MAPENDEKEZO

Utafiti wetu umeshughulikia tu muundo wa kishazi huru arifu. Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusiana na vishazi tegemezi ambapo nafasi ya kijalizi itaonekana kwa uwazi zaidi na vilevile vishazi vilivyo na dhamira tofauti na ile ya uarifu. Tumeonelea kuwa kwa kufanya utafiti kuhusiana na vipengele hivi, mahitimisho ya kijumla yanawezekana kuhusiana na matumizi ya nadharia ya *X-bar* katika lugha ya Kiswahili. Utafiti wetu umejikita katika kuangalia miundo ya virai vichache vya mnyambuliko kutokana na sababu za kiwakati. Tunapendekeza kwamba utafiti zaidi ufanywe kuhusiana na viambishi vingine vya awali vya mnyambuliko wa kitenzi vikiwemo virai vya hali, ukusho na virejeshi. Vilevile ipo haja ya kuangalia sio tu viambishi awali vya mnyambuliko bali pia vile vya tamati kutokana na hali ya kuwa lugha ya Kiswahili ina utajiri wa mnyambuliko.

Mbali na nadharia hii ya *X-bar* kuna nadharia zingine ambazo hazijatumika katika kuchunguza miundo ya lugha ya Kiswahili. Tunatoa changamoto kwa utafiti zaidi

ufanywe kwa kuzingatia nadharia zingine ambazo hazijatumika na vilevile zile  
zinazoibuka ili kuweza kufikia mahitimisho ya kijumla kuhusiana na sarufi ya lugha hii.

# MAREJELEO

- Akmajian A. & wengine (1984). *An Introduction to Language and Communication*  
Cambridge: MIT Press
- Ashton E.O(1944). *Swahili Grammar(Including Intonation)*  
London: Longman.
- Broomfield G.W.(1931) *Sarufi ya Kiswahili*  
Nairobi: Oxford university Press.
- Chomsky N (1957) *Syntactic Structures*  
The Hague: Mouton.
- \_\_\_\_\_ (1965) *Aspects of the Theory of Syntax*  
Cambridge: MIT Press.
- Culicover P.W (1976) *Syntax*  
New York: Academic Press.
- Haegeman L (1994) *Introduction to Government and Binding-Chapa ya Pili*  
Oxford: Blackwell Publishers.
- Horrocks G (1987) *Generative Grammar*  
London: Longman Inc.
- Kamau S.W.(2001) *Sintaksia ya Virai vya Kiswahili Sanifu Kikikuyu cha Kabete-Ulinganishi*  
Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kapinga M (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili*  
Dar es Salaam: TUKI.
- Kariuki A.W (1997) *Sintaksia ya Virai Rejeshi katika Kiswahili Sanifu na Kikikuyu*  
Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kihore na wengine (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu-Sekondari na Vyuvo*  
Dar es Salaam: TUKI.
- Loogman A.(1965) *Swahili Grammar and Syntax*  
Pittsburg: Duquesne University.Press.
- Massamba D.P. & wengine (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*  
Dar es Salaam: TUKI.

- Mathews P.H. (1997) *A Concise Dictionary of Linguistics*  
Oxford: Oxford university Press.
- Matu P.M (1991) *WH-Movement in Kiswahili*  
Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mgalla R.S.(1990) *The Structure of Kiswahili Sentences-A Transformational Generative Approach*  
Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1999) *Mtalaa wa Isimu -Fonetiki, Fonolojia na Mosolojia ya Kiswahili.*  
Nairobi: Longhorn Publishers.
- \_\_\_\_\_ *Sintaksia Pevu-Utangulizi*  
Mswada Ambao Haujachapishwa.
- Mkude J J D (1983) *Uchambuzi wa Sentensi za Kiswahili*  
ktk. Lugha ya Kiswahili: Dar es Salaam.
- Mohamed M.A (2001) *Modern Swahili Grammar.*  
Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Newmeyer F.J (1986) *Linguistic Theory in America 2<sup>nd</sup> edition*  
Orlando: Academic Press Inc.
- Olali T.M (1997) *Kikundi Nomino cha Kiswahili-Mtazamo wa X-bar*  
Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ouhala J.(1991) *Functional Categories and Parametric Variation*  
London: Routledge.
- Polome E.(1967) *Swahili Language Handbook*  
Washinton: Centre for Applied Linguistics.
- Radford A.(1988) *Transformational Grammar*  
Cambridge: Cambridge University Press.
- \_\_\_\_\_ (1997) *Syntax- A Minimalist Introduction*  
Cambridge: Cambridge University Press.
- Schroder H (2001) *Word Order in Toposa-An Aspect of Multiple Feature Checking.*  
Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Sewangi S.(1993) *The Syntax of the Empty Category in the Swahili Simple Sentence.*  
Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi
- Stockwell R.P.(1977) *Foundations of Syntactic Theory*  
NewJersey: Prentice Hall Inc.

TUKI (1990)

*Kamusí Sanifu ya Isimu na Lugha*  
Dar es Salaam: TUKI.

Wesana-chomi E.(1973)

*Towards the Syntax of Complex Sentences in Kiswahili*  
Ktk.Kiswahili Vol.43/2  
Jarida la TUKI: Dar es Salaam.